

Chanjo ya Covid-19
Jua Haki Zako kwa Wanachama wa Jumuiya ya Wahamiaji

- Chanjo inapatikana bila gharama yoyote kwa kila mtu Marekani, bila kujali hali ya uraia (hata kama haujawekwa kwenye stakabadhi). Kadi ya bima inaweza kuombwa lakini haihitajiki ili kupokea chanjo.
- Social security number (Nambari ya usalama wa umma) haihitajiki ili kupata chanjo. Mtoaji akikuuliza social security number na huna au huhisi sawa kuishiriki, unaweza kujibu kuwa huna moja au huhisi sawa kuishiriki.
- Unaweza kuulizwa utambulisho ili kupata chanjo yako. Ikiwa huna kitambulisho cha jimbo/leseni ya dereva, unaweza kuombwa kutoa barua, taarifa, au bili ya matumizi iliyo na anwani yako ya sasa au barua kutoka kwa kanisa, shirika, au mtoaji anayekujua akikiri kuwa unaishi au kufanya kazi katika jimbo la Washington.
- Centers for Disease Control and Prevention (Vituo vya Udhhibiti na Uzuiaji wa Ugonjwa) na Department of Health and Human Services (Idara ya Afya na Huduma za Binadamu) ya Marekani imesisitiza kuwa data ya kibinafsi itatumika tu kwa madhumuni ya afya ya umma. Data ya kibinafsi huenda isitumike kwa mashtaka ya kiraia au kijinai, ikijumuisha utekelezwaji wa uhamiaji.
- Kupata chanjo haitakuwa ada ya umma kwa njia yoyote. Kutumia chanjo hakutazuia nafasi ya kupata ukaaji na/au hali ya uraia.
- Hakuna anayestahili kuuliza kuhusu hali yako ya uhamiaji kwa ajili ya kukupatia chanjo lakini ukiulizwa kuhusu hali yako ya uhamiaji wakati wowote, una haki ya kutojibu.
- Mtu yeyote anaweza kupata chanjo bila kujali hali yao ya uhamiaji. Huhitajiki kutoa uthibitisho wa hali yako ya uhamiaji ili kupata chanjo.

Shukrani za kipekee kwa Legal Counsel for Youth and Children (Mshauri wa Kisheria kwa Vijana na Watoto, LCYC) na Northwest Health Law Advocates (Mwakili wa Sheria ya Afya katika Northwest, NoHLA)

Waraka huu ulihakikiwa na WA Department Of Health (Idara ya Afya, DOH)

